Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Kuunganisha salama.

Majadiliano na watu wachanga kuhusu kuweka data zao na taarifa zao za kibinafsi salama yanafaa kuanza kabla ya wao kwenda mtandaoni. Wanafaa kujua wanavyounganisha kwenye Intaneti: Je, wanatumia muunganisho wa modemu, Wi-Fi au mtandao wa simu (k.m, 4G). Pia wanafaa kufahamu ukosefu wa usalama unaowezekana. Kwa mfano, iwapo mtoto wako anatumia Wi-Fi, wanafaa kufahamu tofauti kati ya mitandao yenye usalama na isiyo na usalama. Miunganisho salama ya Wi-Fi inahitaji nenosiri ili kutumia na kawaida ni salama kuliko mitandao isiyo na usalama. Hata hivyo, wakati mwingine kutumia mtandao wa umma na usio na nenosiri ndiyo njia pekee ya kwenda mtandaoni. Msaidie mtoto wako kujifunza hatua wanazoweza kuchukua ili kulinda taarifa zao wanapounganisha kwenye Intaneti kwa njia hii, kama vile kutumia muunganisho wa VPN uliosimbuliwa.

ANZISHA MAZUNGUMZO KUHUSU KUUNGANISHA SALAMA:

- Huwa unatumia njia zipi kuunganisha kwenye intaneti? Acha tujifunze zaidi kuhusu jinsi njia hiyo hufanya kazi (k.m, tazama video mtandaoni).
- Ni kwa nini unafikiria kwamba kushiriki taarifa za kibinafsi, kama nambari za kadi ya mkopo, kwa mtandao usio salama ni hatari?
- Kwa nini ni muhimu kuwa makini kuhusu kushiriki nenosiri ya Wi-Fi za familia yetu?

Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Pata kitu bora kutoka kwa nenosiri

Nenosiri thabiti ni mojawapo ya njia rahisi zaidi za kulinda taarifa tunazoshiriki mtandaoni. Watu wachanga wanapaswa kujua jinsi ya kuunda moja na kuiweka salama. Msaidie mtoto wako kuunda nenosiri ambalo ni angalau vibambo 7 kwa urefu; linatumia mchanganyiko wa herufi, nambari na ishara zlizotolewa bila utaratibu; na, halina taarifa yoyote ya kibinafsi Nenosiri likiwa ndefu na ngumu, ndivyo litakuwa ngumu kuvunja—japo linaweza kuwa vigumu pia kukumbuka. Njia moja ya kuunda nenosiri ambalo ni rahisi kukumbuka ni kubadilisha baadhi ya herufi za kirai. “I love pasta!” inaweza kuwa nenosiri “1L0v3P*$t*!” Mkumbushe mtoto wako kuepuka kushiriki nenosiri au kuandika pahali.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU NENOSIRI:

- Umewahi kuhisi kushinikizwa ili kushiriki nenosiri lako na mtu? Ulifanya nini?
- Kwa nini ni muhimu kuwa na nenosiri tofauti kwa kila akaunti?
- Acha tujadiliane hali ambapo naweza kuulizia nenosiri lako. Ni vipi tunaweza kuhakikisha kuwa faragha yako inaheshimiwa? Ni vipi tunaweza kuhakikisha nina zana ninazohitaji kuiweka salama?

Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Kuchukua fursa nzuri ya mipangilio ya faragha

Mipangilio ya faragha inaweza kuwasaidia watu wachanga kuchukua baadhi ya udhibiti wa anayeona taarifa zao na pahali ambapo imeshirikiwa. Kwa mfano, baadhi ya majukwaa huruhusu picha kushirikiwa na watu maalum. Ili kuchukua fursa nzuri ya mipangilio ya faragha, watu wachanga wanahitaji kujua hasa ni taarifa gani wanashiriki wakiwa mtandaoni—inaweza kuwa zaidi ya wanavyofikiria. Kwa mfano, baadhi ya majukwaa ya kidijitali yanatumia teknolojia, kama vidakuzi na GPS, kufuatilia shughuli ya wavuti na maeneo halisi ya mtumiaji. Kwa bahati nzuri, nyingi ya majukaa haya yanatoa chaguo la kuzima vipengele hivi (au baadhi yao). Zingatia kumsaidia mtoto wako kufahamu na kutumia mipangilio ya faragha kwa kila jukwaa la kidijitali wanalotumia. Lakini uwakumbushe kwamba mipangilio ya faragha haiwezi kulinda taarifa yao kabisa. Ikiwa wana wasiwasi kuhusu kitu wanachoshiriki mtandaoni kuzidi udhibiti wao, ni vyema wasikishiriki kabisa.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUTUMIA MIPANGILIO YA FARAGHA:

- Ni vipi unatumia mipangilio ya faragha ili kulinda taarifa zako?
- Je, ulijua kwamba picha zinaweza kuwa na metadata zinazoonyesha ni lini na wapi zilichukuliwa? Acha tuone iwapo kifaa/jukwaa lako la kidijitali lina njia ya kuzima hiyo.
- Je, huwa unatumia huduma za kuingia kwenye maeneo? Unachukua hatua zipi kulinda eneo lako kama hutaki kulishiriki?

Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Sheria za kushiriki

Ili kusaidia mtoto wako kufahamu misingi ya kidijitali ya kushiriki taarifa za kibinafsi, wafunze kwamba maudhui ni muhimu. Katika baadhi ya visa, wanaweza kulazimika kushiriki taarifa ili kupata ufikiaji wa baadhi ya programu na tovuti, kama vile majina, anwani za barua pepe na tarehe za kuzaliwa. Katika visa vingine, wanaweza kutaka kushiriki taarifa kuhusu maisha yao, kama vile picha. Mtoto wako anafaa kujua jinsi ya kujua iwapo ombi la taarifa za kibinafsi linatoka kwa jukwaa la kuaminika au mtu binafsi wa kuaminika. Kwa mfano, majukwaa yenye sifa huchukua hatua ili kuweka salama taarifa za mtumiaji na kuwa na sera za faragha zinazoonyesha wanachofanya na taarifa za mtumiaji. Watu binafsi huonyesha kwamba wao ni waaminifu kwa kuheshimu taarifa za kibinafsi zilizoshirikiwa na wao. Hii ni pamoja na kutodhulumu, kutoshiriki bila idhini na vinginevyo kutochukua fursa ya mtumiaji. Mfunze mtoto wako kwamba watu wasioheshimu taarifa zao za kibinafsi hawafai kuzifikia.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUSHIRIKI TAARIFA ZA KIBINAFSI:

- Ni taarifa gani za kibinafsi ambazo unatahadhari kuhusu kuzishiriki mtandaoni?
- Huwa unaangalia vidokezo vipi ili kujua iwapo tovuti/programu/jukwaa ni mwaminifu?
- Ni nini unaweza kufanya iwapo mtu uliyeshiriki taarifa za kibinafsi naye amevunja uaminifu wako?

Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Shughuli za familia

Mipangilio ya faragha

Kujua namna ya kutumia mipangilio ya faragha ni stadi msingi muhimu ya kidijitali kwa kila mtu mchanga. Shughuli hii itamsaidia mtoto wako kufikiria kuhusu aina tofauti za taarifa wanazoshiriki mtandaoni na wanavyoweza kutumia sera za faragha kuilinda.

1. Muulize mtoto wako: **Una udhibiti wa kiasi gani dhidi ya taarifa unayoshiriki mtandaoni?**
2. Msaidie mtoto wako kufikiria kuhusu ni taarifa gani wanaweza kutaka kuweka siri mtandaoni, kama vile nambari ya simu, anwani, ratiba nae neo. Waulize iwapo kuna taarifa yoyote ambayo wangependa kushiriki na baadhi ya watu, kama vile marafiki, lakini si na watu wengine.
3. Mwambie mtoto wako: **Hatuwezi kudhibiti kabisa kinachofanyikia taarifa tunazoshiriki mtandaoni, lakini tunaweza kutumia mipangilio ya faragha kusaidia kuidhibiti. Kwa mfano, baadhi ya mipangilio ya faragha inaweza kukusaidia kudhibiti anayeona taarifa unayochapisha. Acha tuangalie mipangilio ya faragha kwenye wavuti unazopenda.**
4. Mipangilio ya faragha ni tofauti kwenye kila jukwaa na inaweza kuwa ngumu kufahamu. Msaidie mtoto wako kufikiria kuihusu kwa uhusiano na taarifa wanayotaka kudhibiti. Kwa mfano, iwapo mtoto wako anataka kuweka anwani zao za barua pepe siri, wanafaa kutafuta mipangilio inayowaruhusu kudhibiti anayeona taarifa yao ya kibinafsi. Msaidie mtoto wako kuuliza maswali kuhusu kile ambacho mipangilio yao ya faragha inaweza kufanya, kama vile:
   - Je, mipangilio hii ya faragha itaniruhusu kuchagua ni hadhira gani inaweza kuona ninachoshiriki?
   - Ni taarifa gani ya kibinafsi (k.m, taarifa ya mwasilani) mipangilio hii itanisaidia kuweka siri?
   - Je, naweza kudhibiti anayewasiliana nami—ikiwa ni pamoja na watu nisiowajua?
   - Je, naweza kuondoa wasifu wangu kwa utafutaji unaofanywa kwenye kivinjari?
   - Je, naweza kutumia mipangilio hii kuzuia jukwaa dhidi ya kufuatilia eneo langu halisi au vitendo vya mtandaoni?

DOKEZO: Ukiwa na mtoto mdogo, unaweza kutaka kuwasaidia kusoma na kuchagua mipangilio yao ya faragha. Ukiwa na mtoto mkubwa, wanaweza kutaka mipangilio yao ya faragha wao wenyewe—ikiwa ni pamoja na baadhi ya mipangilio inayokuzuia kuwa na ufikiaji kamili kwa maudhui yao. Kila familia itakuwa na sharia tofauti kuhusu ni taarifa gani Watoto wanaruhusiwa kuweka siri kwa watunzaji wao. Zungumza na mtoto wako kwa mapema kuhusu sharia za familia, ikiwa ni pamoja na matokeo ya kuzivunja.

Kuwa Dijitali...kwa Misingi
Shughuli za familia

Nenosiri imara

Nenosiri imara husaidia kulinda taarifa yako ya kibinafsi mtandaoni. Shughuli hii itamsaidia mtoto wako kujifunza jinsi ya kuunda nenosiri imara na linaloweza kukumbukwa.

1. Muulize mtoto wako: **Ni vipi unachagua nenosiri kwa akaunti zako za mtandaoni?**
2. Mwambie mtoto wako: **Nenosiri imara hukusaidia kulinda akaunti zako za mtandaoni. Unadhani nenosiri linafaa kuwa na sifa zipi?**

   Iwapo mtoto wako hajataja sifa zifuatazo, watanguize kwenye mazungumzo yenu. Nenosiri imara:
   - Ni rahisi kukumbuka.
   - Linawekwa kibinafsi. Watu wachanga hawafai kushiriki nenosiri na mtu yeyote isipokuwa watunzaji wao isipokuwa pakihitajika kisheria.
   - Ni vigumu kuakisi. Hayafai kuwa na taarifa ya kibinafsi au inayofahamika vizuri.
   - Lina angalau vibambo 7 kwa urefu. Nenosiri likiwa refu ni bora zaidi.
   - Tumia mchanganyiko wa herufi kubwa na ndogo, nambari na ishara.
3. Kwa kutumia taarifa ya hapo juu, wewe na mtoto wako mnafaa kuunda nenosiri moja imara na moja dhaifu. Elezea kila mmoja kinachofanya nenosiri lenu kuwa imara au dhaifu.

CHANGAMOTO

Huku ukifanya zoezi ya kuunda nenosiri dhabiti, unaweza pia kuchukua nafasi hiyo ili kuongea na mtoto wako kuhusu kanuni, wazo la utatuzi wa shida kutumia kompyuta. Kanuni ni seti ya maelekezo ya hatua kwa hatua yanayotumika kukamilisha kazi. Katika hali hii, kazi ni kuunda nenosiri. Kuunda kanuni inaweza kurahisisha kukumbuka nenosiri kwa sababu kila nenosiri linafuata seti sawa ya kanuni.

MFANO WA KANUNI YA NENOSIRI:

1. Chukua kila herufi nyingine kwenye URL ya website na uziunganishe.
2. Andika herufi za kwanza na za mwisho kwa herufi kubwa.
3. Hesabu herufi hizo na uongeze nambari hiyo katikati ya herufi zilizounganishwa.
4. Hesabu herufi hizo na uongeze ishara zinazofanana mwisho. Kwa mfano, kukiwa na herufi saba, tumia ishara ya “&”. Kukiwa na zaidi ya herusi tisa, ongeza ishara mbili, kwa mfano “12” itakuwa “!@”.
5. Unda sharia moja ya mwisho ya kutumia iwapo nenosiri ni chini ya vibambo 7. Kwa mfano, ongeza nambari unayopenda zaidi pamoja na tatu mwishoni mwa nenosiri.

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Usawa: Haihusu tu muda

Usawa wa kidijitali unazingatia **kiasi** na **ubora** wa muda wa Watoto mtandaoni. Maswali mawili muhimu ya kujiuliza kuhusu kiwango cha muda ambao Watoto wako huchukua mtandaoni ni:

1. "Je, inawazuia watoto wangu dhidi ya kukamilisha majukumu yao?"
2. "Je, inaathiri afya ya kimwili au kihisia ya mtoto wangu?"

Iwapo jibu kwa moja kati ya maswali hayo ni "ndiyo", mtoto wako anaweza kuhitaji vikwazo vikali vya muda mtandaoni. Iwapo jibu kwa moja kati ya maswali hayo ni "la", jiulize kuhusu ubora wa muda wa mtoto wako mtandaoni. Kusaidia watu wadogo kuboresha uhusiano kati yao na watu wengine na kuchunguza matamanio ni mojawapo ya manufaa muhimu ya kusoma mtandaoni.

Unaweza pia kuwasaidia kwa kuunganisha shughuli zao za mtandaoni na matamanio yao ya nje ya mtandao. Kwa mfano, baada ya kutazama klipu ya mchezo wa soka, wewe Pamoja na mtoto wako mnaweza kujaribu kufanya miondoko hiyo mnapocheza mpira nje.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU USAWA:

- Je, huwa unahisi kwamba unatumia muda mwingi sana mtandaoni? Kwa nini au kwa nini hukufanya hivyo?
- Ni shughuli zipi za nje ya mtandao unatamani ungekuwa na muda mwingi wa kuzifanya?
- Ni shughuli zipi za mtandaoni unatamani ungekuwa na muda mwingi wa kuzifanya?

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Usawa: Haihusu tu muda

Usawa wa kidijitali unazingatia **kiasi** na **ubora** wa muda wa Watoto mtandaoni. Maswali mawili muhimu ya kujiuliza kuhusu kiwango cha muda ambao Watoto wako huchukua mtandaoni ni: 1) “Je, inawazuia watoto wangu dhidi ya kukamilisha majukumu yao?” na 2) “Je, inaathiri afya ya kimwili au kihisia ya mtoto wangu?”

Iwapo jibu kwa moja kati ya maswali hayo ni “ndiyo”, mtoto wako anaweza kuhitaji vikwazo vikali vya muda mtandaoni. Iwapo jibu kwa moja kati ya maswali hayo ni “la”, jiulize kuhusu ubora wa muda wa mtoto wako mtandaoni. Kusaidia watu wadogo kuboresha uhusiano kati yao na watu wengine na kuchunguza matamanio ni mojawapo ya manufaa muhimu ya kusoma mtandaoni.

Unaweza pia kuwasaidia kwa kuunganisha shughuli zao za mtandaoni na matamanio yao ya nje ya mtandao. Kwa mfano, baada ya kutazama klipu ya mchezo wa soka, wewe Pamoja na mtoto wako mnaweza kujaribu kufanya miondoko hiyo mnapocheza mpira nje.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU USAWA:

- Je, huwa unahisi kwamba unatumia muda mwingi sana mtandaoni? Kwa nini au kwa nini hukufanya hivyo?
- Ni shughuli zipi za nje ya mtandao unatamani ungekuwa na muda mwingi wa kuzifanya?
- Ni shughuli zipi za mtandaoni unatamani ungekuwa na muda mwingi wa kuzifanya?

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Wewe ni kile unachotazama/shiriki/kuchapisha

Utambulisho wa kidijitali au mtandaoni ni matoleo yetu ambayo yapo mtandaoni. Watu wadogo wanaweza kuwa na utambulisho wa mtandaoni unaofanana na utambulisho wao nje ya mtandao au mpya kabisa. Watu wengine wadogo hubadilisha utambulisho kutegemea wanaowasiliana nao. Kwa mfano, wanaweza kutumia utambulisho mmoja na marafiki na mwingine na familia—ni kawaida. Hata nje ya mtandao, watu wadogo na wazima wanaweza kubadilisha tabia yao wanapowasiliana na vikundi tofauti vya watu. Hata hivyo, walio na fahiwa sawa ya binafsi huonyesha maadili sawa ya kimsingi katika kila mtagusano.

Unaweza kumsaidia mtoto wako kujenga utambulisho dhabiti mtandaoni kwa kufafanua maadili ya kimsingi yaliyo muhimu kwa familia yenu pamoja. Unaweza pia kutaka kuuliza mtoto wako kuhusu maadili waliyounda kutokana na tajiriba zao wenyewe. Zungumza na mtoto wako kuhusu namna ya kutumia maadili yao mfululizo na kuwa halisi kivyao wenyewe mtandaoni, hata ikiwa ngumu na tata.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU UTAMBULISHO WA KIDIJITALI:

- Je, huwa unachapisha kitu mtandaoni kwa sababu unawataka watu wakuone kwa njia fulani?
- Je, yeyote kati ya marafiki zako hutenda tofauti akiwa ana kwa ana zaidi ya wanafofanya mtandaoni? Je, unahisi nini kuhusu hilo?
- Nafahamu kuwa unaweza kuwa na zaidi ya utambulisho mmoja mtandaoni. Je, utakuwa sawa nikiziona zote?

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Weka mpango wa kurudi

Ustadi wa ustahimilivu ni sehemu muhimu ya ustawi wa kidijitali. Unawezesha watu wadogo kudhibiti hali na hisia hasi. Njia moja ya kusaidia mtoto wako kujenga stadi za ustahimilivu ni kujenga mipango ya kukabiliana na hali wanazoweza kukumbana nazo mtandaoni. Kwa mfano, muulize mtoto wako kile wanachoweza kufanya iwapo rika zao walitoa maoni hasi kuhusu picha waliyoshiriki mtandaoni. Wakati wa majadiliano, unaweza kuhalalisha hisia zao huku ukiwasaidia kubuni jibu lisilofanya hali hiyo kuwa mbaya zaidi. Kwa kupitia matukio mapema, unaweza kumsaidia mtoto wako kujiamini zaidi kuwa wanaweza kushughulikia hali yoyote inayotokea mtandaoni.

Kuweza kugundua uhusiano wenye kuauni ni ustadi mwingine muhimu wa ustahimilivu. Kuwa na majadiliano haya huonyesha mtoto wako kwamba upo kwa ajili ya kuwasikiliza na kuwaauni wakiwa mtandaoni.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU USTAHIMILIVU:

- Wakati mwingine nina wasiwasi kuhusu kile ambacho unaweza kukumbana nacho mtandaoni. Je, tunaweza kujadiliana kuhusu baadhi ya hali tofauti na unavyoweza kujibu?
- Je, utahisi sawa kuzungumza nami kuhusu shida zinazoweza kufanyika mtandaoni?
- Tunapohisi hisia kali, inaweza kuwa ngumu kutojibu mara moja. Ni hatua gani hizo unazoweza kuchukua kudhibiti hisia zako kabla ya kutenda?

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Shughuli kwa familia

Kujiandaa kwa ajili ya ustahimilivu

Watu wadogo wanapokumbana na hali ngumu mtandaoni, huenda wasijue namna ya kujibu. Shughuli hii itasaidia mtoto wako kujifunza jinsi ya kufanya uchaguzi sawa mtandaoni kwa kuwahimiza kufikiria kuhusu matokeo yanayoweza kutokana na maamuzi yao.

1. Muulize mtoto wako: **Utahisi vipi iwapo vitu hivi vilikufanyikia ulipokuwa mtandaoni?**
   - Mtu anachapisha picha yako inayokuaibisha.
   - Mtu anachapisha kitu ambacho hukufanya usihisi vizuri, kama vile maoni mabaya kuhusu kikundi cha watu.
   - Mtu anachapisha maoni mabaya kuhusu kitu ulichoshiriki mtandaoni.
   - Mtu anachapisha kitu usichokubaliana nacho. Kwa mfano, wanasema kwamba wimbo unaoupenda ni wa ujinga.

2. Mwambie mtoto wako: **Unaweza kukosa kudhibiti jinsi unavyohisi, lakini unaweza kudhibiti unachofanya na unavyojibu maoni hasi. Unafaa kujaribu kufanya maamuzi yatakayokuwa na matokeo chanya.**

3. Anza stakabadhi kwenye kompyuta au kwa mkono. Katika sehemu ya juu, andika au mtoto wako aandike, **"Mtu au kitu kikinikasiriksha mtandaoni, naweza kuchagua jinsi ya kujibu. Naweza:"**

   Fanya kazi na mtoto wako kufikiria orodha ya vitendo wanavyoweza kufanya. Kisha, pitia orodha hiyo na mjadiliane kuhusu matokeo chanya na hasi ya kila kitendo. Tumia usimbuaji wa rangi au ishara kubainisha vitendo vyenye matokeo chanya na vitendo vyenye athari hasi.

MFANO:

Mtu au kitu kikinikasirisha mtandaoni, naweza kuchagua namna ya kujibu. Naweza:

- Chukua pumzi ya kina au fanya kitu kingine hadi nitulie. Kisha jibu. 😊
- Pata usaidizi kutoka kwa familia na marafiki. 😊
- Jibu kwa kitu kibaya. ☹
- Anza vita mtandaoni ☹
- Izuie au uiripoti. 😊

KUMBUKA: Kitendo kilicho na matokeo chanya yaliyo wazi kwako, kwa mfano, mtoto wako kukukujia kwa sababu ya usaidizi, kinaweza kuonekana tofauti kwa mtoto wako. Baadhi ya watu wengine wadogo wana wasiwasi kwamba kuenda kwa wazazi wao/watoa huduma kwao kutafuta usaidizi kutasababisha matokeo hasi—kupigwa marufuku kutumia tovuti au jukwaa. Mkijaribu kufahamu mtazamo wa kila mmoja, mnaweza kufanya kazi Pamoja ili kutambua matokeo yenye afya zaidi katika kila hali. Kwa mfano, saidia mtoto wako kufahamu kwamba kukuja kwako kutafuta usaidizi hujenga uaminifu na kunaweza kusababisha uhuru mwingi mtandaoni.

Kuwa Kidijitali...na Ustawi
Shughuli kwa familia

Kupangia ustawi wa kidijitali

Stadi za ustawi wa kidijitali zinaweza kuwasaidia watu wadogo kufanya matumizi ya mtandao uwe wenye afya na sehemu yenye usawa kwa maisha yao kwa jumla. Shughuli hii itasaidia mtoto wako kuunda mpango wa hali njema ya kidijitali unaohimiza matumizi yenye afya na usawa.

1. Mwambie mtoto wako: **Ni muhimu kwangu kwamba muda wako mtandaoni ni bora na wenye usawa. Je, tunaweza kufanya kazi pamoja ili kuja na mpango wa kukusaidia kutumia mtandao hivyo?**

2. Chapisha na utumie kurasa za Mpango wa Ustawi wa Kidijitali kumsaidia mtoto wako kuimarisha mpango wa ustawi wa kidijitali. Msaidie mtoto wako kuhisi umiliki wa mpango huo kwa kusikiliza mchango wao kwa miongozo ya mpango huo. Pia, ruhusu mtoto wako aamua athari (iwapo zipo) za kutofuata mpango huo.

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Vidokezo na vianzashaji mazungumzo kwa familia

Jifunze kujenga uhusiano mwema

Kwa watu wengi wachanga, jumuiya za kidijitali ni uenezi wa jumuiya zao za nje ya mtandao. Wanaweza hata kuingiliana na watu kwenye jumuiya zote mbili kwa njia sawa, kama vile kufanya mzaha, kuauni matamanio ya marafiki, kushiriki maudhui, kutengeneza mipango, kubishana na kuchezeana kimahaba. Hata hivyo, kupitia jumuiya za mtandaoni kuna changamoto za kipekee. Inaweza kuweka miingiliano iliyokuwa ya kibinafsi katika nafasi za umma. Kwa mfano, badala ya kutumiana kadi za Siku ya Wapendanao, watu wachanga wanaweza kuweka machapisho ya umma kwa akaunti za mtandao wa kijamii wa kila mmoja. Jumuiya za mtandaoni pia huwapatia watu wachanga ufikiaji wa mfululizo wa kila mmoja, na inaweza kuleta ugumu wa kuheshimu mipaka.

Saidia mtoto wako kupitia jumuiya za mtandaoni kwa njia salama na nzuri kwa kwanza kuongea nao kuhusu uhusiano mwema. Iwapo ni kati ya marafiki, watu wa kawaida unaowafahamu au wengine muhimu, uhusiano mwema unajengwa kwa hisia-mwenzi na heshima. Msaidie mtoto wako kuzingatia jinsi watu wengine wanaweza kuhisi kabla ya kusambaza, kuchapisha au kutoa maoni katika maudhui mtandaoni. Wape mifano ya jinsi heshima inakaa mtandaoni: kutotoa maoni mabaya, kutochapisha picha za wengine bila ruhusa yao, na kutoshiriki gumzo, barua pepe au maudhui mengine yaliyoshirikiwa kibinafsi. Zungumza na mtoto wako kuhusu jinsi ya kuweka mipaka hii na mingine katika uhusiano wao wa mtandaoni. Waelezee kuwa uhusiano ambapo mtu mwingine hawahudumii kwa hisia-mwenzi au heshima si mwema.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU UHUSIANO MWEMA:

- Unawezaje kufafanua uhusiano mwema kati ya marafiki? Je, ufafanuzi wako unabadilika iwapo ni uhusiano wa kimapenzi?
- Je, una marafiki wowote wanaokutumia ujumbe mara nyingi sana? Acha tujadiliane baadhi ya njia za kushughulikia hiyo. Kwa mfano, unaweza kuwaambia kwamba sitaki mpokee ujumbe wakati wa chakula cha jioni.
- Je, marafiki zako hujibu vipi unapowaomba wasisambaze picha zako mtandaoni? Huwa unafanya nini wasiposikiliza?

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Vidokezo na vianzashaji mazungumzo kwa familia

Kumbuka kuthibitisha

Watu wengi wanatumia jumuiya zao za mtandaoni kama chanzo cha taarifa. Hata hivyo, si taarifa yote inayoshirikiwa ni sahihi. Inaweza kuwa ngumu kwa mtu yeyote, ikiwa ni pamoja na watu wachanga, kujua ni taarifa gani wanafaa kuamini. Hii ndiyo sababu sehemu muhimu ya uhusiano wa kidijitali na kujenga jumuiya nzuri za mtandaoni ni kuthibitisha maudhui kabla ya kushiriki. Raia wa kidijitali wakijua kwamba wanaweza kupata taarifa yenye sifa nzuri katika jumuiya ya kidijitali, huwa inasaidia katika kujenga uaminifu. Mfunze mtoto wako kuuliza maswali matano ya uthibitisho kabla ya kuamini au kushiriki maudhui mtandaoni: **(1)** Maudhui hayo yalitoka wapi? **(2)** Ni nani aliunda maudhui hayo? **(3)**Yaliundwa lini? **(4)** Yaliundwa wapi? **(5)** Yaliundwa kwa nini?

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUTHIBITISHA TAARIFA:

- Kuna tofauti gani kati ya maoni na ukweli?
- Je, umewahi kuamini kitu ulichosoma mtandaoni, kisha kugundua baadaye kwamba ni uwongo? Ulifanya nini?
- Je, una marafiki wowote wa mtandaoni wanaoshiriki taarifa nyingi zisizo za ukweli? Unahisi vipi kuhusu hilo?

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Vidokezo na vianzashaji mazungumzo kwa familia

Waongoze kwa hisia-mwenzi

Miingiliano ya mtandaoni inaweza kukosa ishara za kijamii zinazoweza kutusaidia kuamua jinsi watu wengine wanahisi tukiwa ana kwa ana. Bila ishara hizi, baadhi ya watu wachanga wanaweza kusahau kwamba kuna mtu mwingine anayesoma na anakuwa na jibu la kihisia kwa maudhui wanayoshiriki mtandaoni. Kuwahimiza watu wachanga kuwa na hisia-mwenzi kunaweza kusaidia katika kupunguza dhuluma mtandaoni kwa kuwasaidia kufikiria kuhusu hisia za watu wengine. Anza kwa kumfunza mtoto wako kutulia kabla ya kuchapisha maudhui mtandaoni. Wanafaa kujiuliza: “Je, nataka watu wahisi vipi kuhusu maudhui yangu?” na “Ni nani anaweza kuumizwa na maudhui haya?” Mkumbushe mtoto wako kwamba wanavyowahudumia watu mtandaoni haufai kuwa tofauti na wanavyofaa kuwahudumia nje ya mtandao.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU HISIA-MWENZI:

- Je, mtu yeyote amewahi kuelewa vibaya kitu ulichochapisha mtandaoni? Ulijibu vipi?
- Unafikiri ni kwa nini watu husema mtandaoni vitu ambavyo hawawezi kusema ana kwa ana?
- Umewahi kusoma mtandaoni maoni mabaya kuhusu mmoja wa marafiki zako? Yalifanya uhisi vipi? Ulifanya kitu chochote?

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Vidokezo na vianzashaji mazungumzo kwa familia

Kuwa raia wa kidijitali mwenye kujituma.

Uhusiano wa kidijitali unahitaji kitendo. Watu wachanga hawatakuwa na jumuiya nzuri mtandaoni isipokuwa wakichukua vitendo chanya na kukataa vitendo hasi. Iwapo mtoto wako atamwona mtu akichokozwa au akinyanyaswa mtandaoni, wasaidie kupata njia waliyo sawa nayo na kutoa usaidizi. Wanaweza kushiriki ujumbe wa kibinafsi au wa umma wa usaidizi au kauli ya jumla unaowahimiza watu kuwa wakarimu mtandaoni. Mtoto wako pia anafaa kuwa makini kwa taarifa yoyote inayoshirikiwa katika jumuiya yao ya mtandaoni inayoweza kuwa ya sifa nzuri au sahihi. Wanaweza kuchukua hatua kuthibitisha taarifa hiyo na kisha kushiriki matokeo na jumuiya hiyo huku bado wakiwa na heshima kwa mchapishaji asili.

Msaidie mtoto wako kujituma kuunda kitendo chanya mtandaoni. Kwa kuwa karimu na kuonyesha huruma katika shughuli zao za kila siku mtandaoni, wanaweza kusaidia kuthibitisha kwamba kuwa mtu wa kuauni na kuwaleta watu Pamoja ndiyo kawaida katika jumuiya yao ya mtandaoni. Mtoto wako pia anaweza kufanya kazi na marafiki zake nje ya mtandao kuhimiza tabia chanya. Kwa mfano, rafiki akishiriki kwamba wanapanga kumdhulumu mtu mtandaoni, mtoto wako anaweza kuwahimiza kufanya chaguo tofauti.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUWA RAIA WA KIDIJITALI ANAYEJITUMA:

- Utafanya nini ukiona mtu akichokozwa mtandaoni?
- Unaweza kuchukua vitendo vipi kuwahimiza watu kuwa karimu kwenye jumuiya yako ya mtandaoni?
- Utajibu vipi iwapo mtu alikuwa anashiriki taarifa isiyo sahihi mtandaoni kwa bahati mbaya? Na iwapo hawataitoa, hata baada ya wewe kuwaambia kuwa haikuwa sahihi?

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Shughuli kwa familia

Kujenga hisia-mwenzi

Watu wanapozungumza ana kwa ana, tunatumia ishara za jamii kama vile toni ya sauti na ishara ya uso kufahamu kila mmoja. Katika miingiliano ya mtandaoni, ishara hizi hazipo, na inaweza kusababisha kuelewana visivyo. Shughuli hii itasaidia mtoto wako kufikiria kuhusu kile ambacho watu wengine wanamaanisha wanapochapisha maudhui mtandaoni.

1. Mwambie mtoto wako: **Anaposoma maudhui ambayo mtu amechapisha mtandaoni, ni muhimu kutodhani mabaya zaidi. Husaidia kutumia hisia-mwenzi. Jaribu kujiweka katika hali ya mtu huyo na ufikirie hoja wan-ayojaribu kutoa.**

2. Chagua mbinu ya midia ya mtandaoni inayowaruhusu watu kutoa maoni, kama vile gazeti la Makala au blogu la mtandaoni, na usome maoni ambayo watu wamechapisha. Unaweza pia kutumia kitengo cha barua kwa mhariri cha gazeti. Mtoto wako azingatie toni ya sauti ambayo mwandishi wa maoni angetumia iwapo waliyazungumza kwa sauti. Jaribu kusoma maoni katika toni ya sauti tofauti kuona iwapo inabadilisha maana.

CHANGAMOTO

Muulize mtoto wako zana ambazo watu wanatumia mtandaoni kuonyesha hisia, kama vile emoji, mizaha na herufi kubwa. Jaribu kutumia sentensi sawa kuonyesha hisia tofauti kwa kutumia ishara za hisia za mtandaoni. Kwa mfano, maana ya sentensi “napenda nywele zako” hubadilika vipi ikiwa a) herufi kuza zote; b) kando ya emoji ya kupepesa jicho; c) imeshirikiwa kama manukuu ya picha ya mtu aliye na nywele mbaya?

Kuwa Dijitali...na Uchumba
Shughuli kwa familia

Kupata vyanzo vyenye sifa zaidi

Kushiriki taarifa kutoka vyanzo vyenye sifa zaidi ni sehemu muhimu ya kujenga uaminifu katika jumuiya za mtandaoni. Shughuli hii itamsaidia mtoto wako kujifunza jinsi ya kuthibitisha vyanzo vya taarifa wanayopata mtandaoni.

1. Muulize mtoto wako: **Unapoona taarifa mtandaoni, huwa unashangaa iwapo ni ya kweli?**

2. Mwambie mtoto wako: **Ni muhimu kutathmini chanzo cha taarifa hiyo kuona iwapo ina sifa n ani ya kuaminika. Chanzo ni mtu, kampuni au shirika ambalo hushiriki taarifa. Unaposhiriki taarifa mtandaoni, unakuwa chanzo nawe pia. Iwapo unataka kuwa wa kuaminika, utajaribu kushiriki taarifa sahihi kutoka wavuti muhimu.**

3. Tembelea wavuti au jukwaa ambalo wewe au mtoto wako hutumia kupata taarifa. Chagua makala, blogu au sehemu ya maudhui yenye taarifa ili kutazama Pamoja. Chapisha na utumie karatasi ya Njia 5 za Kuthibitisha ili kuitathmini.

4. Baada ya kukamilisha karatasi ya orodha, zingatia kumsaidia mtoto wako kuunda kitu cha kuwakumbusha kuthibitisha vyanzo vya mtandaoni. Kwa mfano, wanaweza kutengeneza bango la maswali 5 ya uthibitisho ili kupachika kwenye chumba chao au picha ya kidijitali ili kutumia kama picha ya mandharinyuma ya kipatakilishi au simu ya rununu.

Kuwa Dijitali...kwa Uwezeshaji
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Fanya utafiti wako

Kabla ya kutetea suala lolote, watu wachanga wanafaa kutumia Intaneti kutafiti mada hiyo. Wavavyozidi kuwa na ufahamu kuhusu kusala hilo, ndivyo wanavyoweza kuwasiliana kwa ufaafu mtandaoni na nje ya mtandao. Kufanya utafiti wa suala hilo kunaweza pia kuwaleta Pamoja na washikadau muhimu. Hawa wanaweza kuwa watu wengine kwenye jumuiya wanaojali suala hilo au wafanya uamuzi wanaoweza kusaidia kuthibitisha suluhisho yoyote. Wanapofanya utafiti, watu wachanga pia wanaweza kukutana na wengine walioshughulikia masuala sawa kwenye jumuiya zao. Watu wachanga wanaweza kulinganisha suluhu hizi ili kukidhi mahitaji yao au kupata ushauri kutoka kwa mawakilishi wao kuhusu namna ya kufaulu. Watu wachanga pia wanafaa kutumia uraia wao wa kidijitali hapa—watahitaji kuthibitisha taarifa zao kabla ya kuchukua hatua yoyote.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUFANYA UTAFITI WA SUALA HILO:

- Ni taarifa gani unahitaji kabla ya kutetea suala?
- Tunaweza kutaka kuwasiliana na nani kuhusu suala hili (k.m, bodi za shule, mabaraza ya jiji)? Unadhani tunaweza kupata taarifa zao za mawasiliano mtandaoni?
- Ni vipi tunajua kwamba taarifa hii ni kutoka kwa chanzo maarufu? (Dokezo: Tumia maswali 5 ya uthibitisho yaliyotajwa kwenye Uhusiano wa Kidijitali)

Kuwa Dijitali...kwa Uwezeshaji
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Jua zana hizo

Kuwasaidia watu wachanga kutumia zana za kidijitali kwa mabadiliko chanya huanza kwa kujua ni zana gani na kufahamu jinsi zinaweza kutumika. Kwa mfano, miraha ya Intaneti huruhusu watu kutumia utamaduni maarufu kama msingi wa kusambaza mawazo yao wenyewe. Iwapo mtoto wako anapendelea kuleta umakinifu kwenye suala, wanaweza kutumia mzaha kuleta ufahamu. Alama za reli ni zana nyingine ya kidijitali ambayo watu wachanga wanaweza kutumia kuongeza sauti zao za mtandaoni. Alama za reli husaidia watu kupanga mawazo sawa chini ya istilahi moja ya utafutaji inayoweza kupatikana kwa urahisi mtandaoni. Hata kama hauko tayari kwa mtoto wako kuunda mizaha na alama za reli zao wenyewe, wanaweza kutumia zana nyingine za kidijitali kujifunza kuhusu kazi inayofanywa tayari kuhusu kisa chao. Kwa mfano, wanaweza kutumia alama za reli kufikia watu, matukio na nafasi za kujitolea zinazohusiana na masuala yao.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUTUMIA ZANA ZA UWEZESHAJI:

- Je, unajali kuhusu masuala gani? Ni vipi unaweza kutumia intaneti na mtandao wa kijamii kusaidia kuyatatua?
- Tutumie alama ya reli kujifunza mengi kuhusu (suala la mtoto wako).
- Ni mizaha gani unapenda zaidi kwenye intaneti? Je, inaweza kusaidia kuongeza ufahamu wa (suala la mtoto wako)?

Kuwa Dijitali...kwa Uwezeshaji
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Toa usaidizi

Watu wachanga wa umri wote wanaweza kupendelea kutatua shida kwenye jumuiya zao. Hata hivyo, mtandao wa kijamii si zana sahihi kiumri kwa Watoto wote. Majukwaa mengi ya mtandao wa kijamii yana mahitaji ya umri ili kusaidia katika kuwalinda watumiaji wadogo. Hii haimaanishi kwamba mtoto wako hawezi kutumia nguvu ya Intaneti kutatua masuala yao. Unaweza kutumia uwepo wako binafsi wa mtandaoni kumsaidia mtoto wako kuleta ufahamu kwenye suala lao. Kwa mfano, unaweza kujiunga na jumuiya ya mtandaoni inayolenga suala la ambalo mtoto wako anapendelea. Hii itapatia mtoto wako nafasi ya kujifunza mengi kuhusu suala hilo, huku ikikupa nafasi ya kuhakiki maudhui na kuchunguza wasilani. Ukiwa amilifu kwenye mtandao wa kijamii, unaweza kutaka kutumia mitandao yako kukuza alama ya reli, mzaha au maudhui mengine ambayo mtoto wako aliunde kuhusu suala lao. Ushiriki wako humpa mtoto wako usaidizi na ulinzi huku wakijaribu kuleta mabadiliko chanya duniani.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUANUNI UANAHARAKATI WA MTOTO WAKO:

- Ni vipi naweza kukusaidia kusambaza neno kuhusu (suala la mtoto wako) mtandaoni?
- Je, kunazo jumuiya za mtandaoni tunazoweza kujiunga nazo ili kujifunza mengi kuhusu (suala la mtoto wako)?
- Acha tuunde (alama ya reli, picha, mzaha, nk.) ninayoweza kushiriki na marafiki zangu ili kusaidia watu kujifunza mengi kuhusu (suala la mtoto wako).

Kuwa Dijitali...kwa Uwezeshaji
Shughuli kwa familia

Kutumia alama za reli

Watu wachanga wanaweza kutumia alama za reli kujifunza au kushiriki kuhusu masuala na visa vya kijamii wanavyotaka kushughulikia. Shughuli hii itamsaidia mtoto wako kujifunza mengi kuhusu jinis alama za reli hufanya kazi na zinavyoweza kutumika kuhimiza wema wa kijamii.

1. Anza kwa kuhakikisha kuwa mtoto wako anajua kutumia alama ya reli ni nini: Matumizi ya alama ya reli kusaidia kupanga taarifa kuhusu mada maalum, na kurahisisha kuipata mtandaoni. Iwapo mtoto wako ametumia alama za reli, waulize ni gani hizo.

2. Mwambie mtoto wako: **Watu wengine hutumia alama za reli kuleta ufahamu wa shida wanazotaka kutatua.**

3. Shiriki baadhi ya njia ambazo watu wameshatumia kwa wema wa kijamii. Zungumza kuhusu kampeni ya ufahamu wa kijamii kwenye jumuiya yako au tumia mojawapo ya mifano hapo chini:
   - #ALSIceBucketChallenge: Alama hii ya reli ilianza 2014 na inatumika kueneza ufahamu kuhusu ALS na kuchangisha pesa ya kutafiti ugonjwa huo.
   - #stopbullying, #bullying, nk.: Watu wa umri wote wanatumia alama za reli zilizo na neno “kudhulumu” kuleta ufahamu kuhusu dhuluma na kuwahimiza watu kuikomesha.
   - #HeForShe: Emma Watson, mtu mashuhuri alianza kutumia alama hii ya reli mwaka wa 2014 kuleta usawa kwa wanawake duniani.

4. Muulize mtoto wako: **Je, kuna masuala yoyote kwenye jumuiya yetu ambayo unataka watu wawe makini kuyahusu?**

5. Msaidie mtoto wako kupata picha inayohusiana na suala lao. Kisha, buni alama mbili au tatu za reli kwa picha itakayosaidia kuleta ufahamu wa suala la mtoto wako. (Kumbuka: Kabla ya kutafuta picha, ona iwapo kivinjari chako kina zana za kukusaidia kuchuja maudhui yasiyofaa na kupata picha zenye haki sawa za matumizi.)

CHANGAMOTO

Iwapo mtoto wako yuko sawa na wazo hilo, zingatia kushiriki alama za reli mtandaoni au nje ya mtandao. Kwa mfano, unaweza kuzichapisha kwenye wasifu wako wa mtandao wa kijamii. Zingatia kupatia kila alama ya reli nambari na kuruhusu mtandao wa mtandao wako wa kijamii kupigia kura kipendwa chao.

Kuwa Dijitali...kwa Uwezeshaji
Shughuli kwa familia

Mbio ya utafiti

Watu wachanga wanaweza kutumia Intaneti kujifunza kuhusu vyanzo wanavyojali. Shughuli hii huwasaidia watu wachanga kujifunza mengi kuhusu jinsi ya kufanya utafiti wa masuala wanayotaka kushughulikia.

1. Zungumza na mtoto wako kuhusu vyanzo wanavyopendelea na kuamua kuhusu chanzo kimoja cha kufanyia utafiti.
2. Muulize mtoto wako ni taarifa gani itakuwa muhimu kujifunza kuhusu kisa chao. Wazia istilahi za utafutaji unazoweza kutumia kutafuta taarifa, ikiwa ni pamoja na alama za reli. Huku ukifanya utafiti, jaribu kupata:
   - Maelezo rahisi kuhusu suala hilo, ikiwa ni pamoja na:
     - Lilivyoanza (iwapo ni muhimu).
     - Linavyoathiri watu.
     - Limewaathiri watu wangapi.
   - Jina la mtu mmoja au wawili wanaofanya kazi kutatua suala hilo.
   - Kampeni ya mtandao wa kijamii inayoleta ufahamu wa suala hilo.
   - Tukio kuhusu suala hilo kwenye jumuiya yako.
3. Msaidie mtoto wako kutathmini kila chanzo kwa kutumia hatua 5 za uthibitisho: **(1)** Maudhui hayo yalitoka wapi? **(2)** Ni nani aliunda maudhui hayo? **(3)** Yaliundwa lini? **(4)** Yaliundwa wapi? **(5)** Yaliundwa kwa nini?

   Mtoto wako anafaa kutumia mbinu ya kuangalia mara tatu kuangalia ukweli kwa ajili ya usahihi: Iwapo taarifa sawa imerudiliwa na angalau vyanzo vitatu vya kuaminika, huwa ni sahihi.
4. Utafiti wako ukikamilika, muulize mtoto wako achague mbinu ya kushiriki taarifa hiyo ama mtandaoni au nje ya mtandao. Kwa mfano, wanaweza kutengeneza bango, kuunda alama ya reli, kuandika wimbo au filamu ya PSA.

Kuwa Dijitali...kwa Nafasi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Himiza ujasiriamali

Stadi za nafasi za kidijitali zinaweza kuwasaidia watu wachanga kujiandaa kujiunga na kazi ya kesho: Pia wanaweza kuwaandaa watu wachanga kuiongoza. Msaidie mtoto wako kujiona kama muundaji sawa na mtumiaji wa teknolojia ya kidijitali. Anza kwa kumkumbusha mtoto wako kuwa kila teknolojia tunayofurahia leo haikuwepo kwa wakati mmoja-mtu alilazimika kuiunda. Kisha utafute hadithi kuwahusu watu wachanga waliounda majukwaa mapya au walitumia teknolojia ya kidijitali kutafuta suluhisho ya uhunifu kwa matatizo yao. Msaidie mtoto wako kujifunza mengi kuhusu kazi zinazolingana na matamanio yao na stadi ambazo wangehitaji kufaulu. Kwa mfano, iwapo mtoto wako anapenda sanaa, wanaweza kuwa na nia ya kuanzisha shirika lao la muundo wa sanaa ya michoro.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU UJASIRIAMALI WA KIDIJITALI:

- Je, unafikiria kuwa watu wachanga wanaweza kuendesha biashara zao wenyewe? Kwa nini au kwa nini hukufanya hivyo?
- Iwapo ulianza biashara yako, inaweza kuwa nini? Ni vipi utatumia Intaneti kujisaidia?
- Iwapo ungejenga program yako binafsi, ingekuwa kuhusu nini?

Kuwa Dijitali...kwa Nafasi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Tetea ufikiaji wa stadi za kusoma na kuandika za kidijitali

Shule nyingi wanataka kuwasaidia wanafunzi wao kujifunza stadi za kusoma na kuandika kidijitali, lakini huenda hawana rasilimali za kutoa maelekezo yenye ubora wa juu. Unaweza kutetea haki ya elimu ya mtoto wako kuhusu teknolojia ya kidijitali. Anza kwa kuuliza shule ya mtoto wako kile ambacho inafanya kuandaa wanafunzi wake kuchukua fursa ya nafasi za siku zijazo katika teknolojia. Wana rasilimali zipi? Je, masomo kuhusu Intaneti, kusoma na kuandika kidijitali na teknolojia ni sehemu ya wastani ya mtaala wa mtoto wako? Ikiwa ni la, tafuta ni kwa nini. Hii itakusaidia kujua jinsi ya kutetea bora zaidi mtoto wako—iwapo ni kuwasiliana na maafisa ili kupata rasilimali zaidi au kuleta mabadiliko katika mtaala wa shule hiyo. Pia unaweza kutolea shule yako suluhisho. Mpango wa “Kuwa Dijitali” ni mojawapo tu ya rasilimali nyingi, mara nyingi bila malipo, zinazopatikana ili kuwasaidia walimu kuleta masomo kuhusu teknolojia madarasani mwao. Shiriki mipango hii na shule ya mtoto wako na, hakikisha kuwa mtoto wako anapokea maarifa anayohitaji ili kufanikiwa katika siku zijazo za kidijitali.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU UFIKIAJI NA SHULE YAM TOTO WAKO:

- Ni rasilimali zipi za kiteknolojia (k.m., kompyuta za eneokazi au kipatakilishi, kompyuta bapa au bao nyeupe) zinapatikana kwa mtoto wako?
- Walimu wanaunganisha vipi matumizi ya teknolojia kwa kazi za ziada za mtoto wangu?
- Je, mtoto wangu wanafundishwa kusoma na kuandika kidijitali na stadi za utatuzi wa shida kutumia kompyuta?

Kuwa Dijitali...kwa Nafasi
Vidokezo na vianza mazungumzo kwa familia

Kuwa mdadisi

Sisi sote si magwiji wa teknolojia ya kidijitali, na hiyo ni sawa. Ukiunda mtazamo wazi na wa kutaka kujua dhidi ya kujifunza stadi za teknolojia, mtoto wako atahimizwa kujifunza kuihusu pia. Acha mtoto wako ajue kwamba unadhani stadi hizi ni muhimu na, tenga muda ya nyinyi wawili kujifunza kwa pamoja. Kwa mfano, mnaweza kutazama video zinazofafanua utatuzi wa shida kutumia kompyuta ili kujifunza mengi kuihusu na stadi zinazohusiana, kama kuchanganua data na kuunda kanuni. Pia unaweza kumuuliza mtoto wako kukufunza kuhusu wanchosoma shuleni. Kitendo cha kukifafanua kitawasaidia kupitia stadi hizo na kufahamu kwa kina zaidi.

ANZA MAZUNGUMZO KUHUSU KUJIFUNZA STADI ZA KIDIJITALI:

- Je, unapendelea kujifunza stadi zipi za kidijitali?
- Je, kunazo stadi zozote za kidijitali unazodhani nafaa kujifunza kuhusu?
- Acha tutazame video kuhusu (k.m, usimbaji, utatuzi wa shida kutumia kompyuta, kanuni, n.k.).

Lengo la zoezi hili ni kujifunza jinsi kanuni ipo kwa usahihi. Iwapo mhandisi wa programu hajajumuisha kila hatua hasa, kanuni hiyo bila shaka haitafanya kazi.

Kuwa Dijitali...kwa Nafasi
Shughuli kwa familia

Kanuni ni nini?

Kanuni ni seti hasa ya maelekezo yanayoweza kutumika kukamilisha kazi. Shughuli hii itamsaidia mtoto wako kufahamu mengi kuhusu jinsi kanuni hufanya kazi na jinsi ya kuziunda.

1. Mwambie mtoto wako: **Kanuni ni seti maelekezo ya hatua kwa hatua ya kukamilisha kazi. Huwa tunafikiria kuzihusu kwa njia ya kompyuta, lakini bila shaka unatumia kanuni bila kugundua. Ni lini ulifuata maelekezo na kukamilisha kazi?**
2. Mwambie mtoto wako: **Malekezo ya mapishi na maelekezo ya kujenga samani ni baadhi ya mifano ya kanuni. Acha tuunde kanuni yetu wenyewe kwa kitu ambacho huwa tunafanya nyumbani.**
3. Acha mtoto wako achague kazi ya kawaida katika nyumba yako kama kutandika kitanda, kufua au kukunja nguo, kupika mlo au kuandaa meza. Waulize kuandika hatua zote zinazohitajika kukamilisha kazi kwa njia sahihi.
4. Mtoto wako akikamilisha, waambie wasome hatua hizo kwa sauti huku ukifuatilia. Hakikisha umefuata hatua hizo **sawasawa**. Kwa mfano, iwapo kazi ni kupika kitu, lakini mtoto wako hajakuambia ufungue viambato, fuata maelekezo yao ukitumia kontena zisizofunguliwa. Mtoto wako ataona kwamba anakosa hatua!
5. Ukimaliza kufuata maelekezo ya mtoto wako, waulize iwapo kazi hiyo ilikamilika sahihi. Iwapo haikukamilika sahihi, waambie waongeze hatua au vinginevyo kuhariri maelekezo yao kukusaidia kukamilisha kazi hiyo. Waambie wasome maelekezo hayo tena huku ukifuatilia. Endelea hadi kanuni ya mtoto wako ikuongoze hadi mwisho wa kazi hiyo kwa usahihi.

CHANGAMOTO

Iwapo mtoto wako anapendelea uchunguzi zaidi wa kanuni, jaribu shughuli “Manenosiri Imara” katika kitengo cha Misingi ya Kidijitali.